



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَكُفَّارُهُمْ بِمَا اسْتَعْلَمُوا لِيَسْتَخْلِفُوهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفْتُ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَإِنَّكُمْ مُّمَكِّنُونَ إِنَّمَا أَرْضُنَا مُّكَفَّرُوْهُمْ وَلَيَسْبِئُنَّهُمْ مِّنْ بَعْدِ حَرْقَهُمْ أَنَّهُ
يَعْدُونَنِي لَا يُنْتَكُونُ بِإِشْيَاءٍ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Jumapili, 6 Jumada II 1446 H

08/12/2024 M

Na: H.T.L 1446 / 07

Taarifa kwa Vyombo vyaa Habari
Kuanguka kwa Utawala Dhalimu nchini Syria ni Furaha kwa Wanyonge
(Imetafsiriwa)

Tunawapongeza Waislamu kwa jumla na watu wa Ash-Sham na Lebanon haswa kwa kuanguka kwa dhalimu wa ash-Sham, Chama cha Baath, familia ya Al-Assad, wapambe wao, majasusi wao na wapumbavu wao, ambaye aliwafanya Waislamu kuonja maovu ya mauaji, mateso, mauaji, kukamatwa na kufurushwa... nchini Lebanon na Syria.

Mnamo Disemba 8, 2024, Bashar aliwakimbia wanamapinduzi na utawala wake wa dhulma ukafikia mwisho. Ni wakati wa kuwaadhibu wahalifu. Waislamu wana haki ya furaha kubwa, na furaha yetu haitakamilika isipokuwa kwa kutabikisha sheria ya Mwenyezi Mungu na kuziunganisha nchi za Waislamu.

Enyi Watu Wetu nchini Lebanon: Nyinyi ni sehemu ya Ash-Sham na ardhi za Waislamu, na wapumbavu wa dhalimu wa ash-Sham daima wamekufedhehesheni kama walivyowafedhehesha watu waliokimbia makaazi yao wa Palestina. Umefika wakati sasa wa nyinyi kukukuta vumbi la udhalilifu na kuungana katika kuwakabili maadui zenu wanaokuvizioni, kuanzia umbile la Kiyahudi, hadi walinzi wake mionganoni mwa watawala, hadi mabwana zao wa Magharibi.

Sisi katika Hizb ut Tahrir/Wilayah Lebanon tunakuhimizeni mushirikiane nasi katika kutimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ya kuhuisha maisha kamili ya Kiislamu kuititia kusimamisha Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, ambayo itatawala kwa Uislamu na kuubeba dunia nzima. Siku hiyo Waumini watafurahia ushindi wa Mwenyezi Mungu, na kuregeshwa kwa chombo cha Ummah kutakuwa ni afueni kwa Waislamu na wengineo. Kama ambavyo kila mtu alifurahia haki zake chini ya Khilafah kwa mamia ya miaka, ikiwa ni pamoja na usalama, amani, kuhifadhi mali, elimu, matibabu, na uchungaji, atafurahia hayo chini ya dola yenu, Khilafah Rashida kwa njia ya Utume.

Mamlaka za Lebanon lazima zichukue hatua ya kuwaachilia huru wafungwa wa Kiislamu kutoka Gereza la Roumieh na jela za Lebanon ambao walikuwa wamefungwa kwa dhulma na kwa ukali, bila ubaguzi, kwa tuhuma za kuunga mkono mapinduzi ya Ash-Sham ili furaha ya Waislamu wa Lebanon ipate kuwa furaha isiyo na kifani.

[وَنَرِيدُ أَنْ تُؤْمِنَ عَلَى الَّذِينَ اسْتَصْبَعُوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلُهُمْ أَنَّمَّةً وَنَجْعَلُهُمُ الْوَارِثِينَ]

“Na tukataka kuwafadhili walio dhoofishwa katika nchi hiyo na kuwafanya wawe waongozi na kuwafanya ni warithi.” [Al-Qasas 28:5]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Lebanon**